THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF FINANCE

MILLENNIUM CHALLENGE ACCOUNT – TANZANIA

HOTUBA YA AFISA MTENDAJI MKUU KATIKA SHUGHULI YA UTIAJI SAINI WA MKATABA WA MRADI WA UJENZI WA BARABARA TANO ZA VIJIJINI PEMBA (KILOMITA 35) 18.08.2011 – WETE, PEMBA

Mgeni Rasmi,

Mheshimiwa Hamad Masoud, Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

Mheshimiwa Alfonso Lenhardt, Balozi wa Marekani

Mheshimiwa Omar Kombo, Mkuu wa Wilaya ya Wete na kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba

Ndugu Karl Fickenscher, Mkurugenzi Mkaazi wa Millennium Challenge Corporation na Mjumbe wa Bodi ya Millennium Challenge Account - Tanzania

Ndugu Khamis Omar, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ambaye pia ni Mjumbe wa Bodi ya Millennium Challenge Account – Tanzania

Dr. Vuai Lila, Katibu Mkuu, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano

Waheshimiwa Wakuu wa WIlaya

Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi

Ndugu Msanif Mussa, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano

Ndugu Abdi Faki, Naibu Katibu, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo

Maafisa Waandamizi wa Serikali na Taasisi

Ndugu Joseph Schwartzman, Afisa Mtendaji Mkuu wa kampuni ya H Young & Co. (East Africa) Limited

Wawakilishi wa Wananchi kutoka Barabara Tano za Mradi

Ndugu Wananchi na Wageni Waalikwa,

Mabibi na Mabwana

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,
Awali ya yote, kwa niaba ya Kitengo cha Millennium Challenge Account - Tanzania (MCA-T) ningelipenda kuitumia nafasi hii kukushukuru Mgeni Rasmi kwa kuamua kuwa nasi katika siku hii muhimu kwa wananchi wa Pemba. Ningelipenda pia nimshukuru sana Mheshimiwa Balozi wa Marekani kwa kuamua kwake kuziacha shughuli zake nyingine muhimu ili kupata nafasi ya kujumuika nasi hapa Wete, Pemba. Hii inaonyesha uzito ambao Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Marekani unaoupa mradi huu muhimu kwa maendeleo ya wananchi wa Pemba.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,
Baada ya kazi ngumu ya kupembua na kuchanganua, leo tumefikia hatua ya utiaji saini wa Mkataba wa Mradi wa Ujenzi wa Barabara Tano za Vijijini Pemba zenye urefu wa kilomita 35 zilizoko katika Mkoa wa Kaskazini.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,
Vile vile, kwa moyo mkunjufu kabisa ningelipenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa uongozi wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba kwa makaribisho na maandalizi ya hali ya juu kama sote tunavyoshuhudia hapa ili kuifanikisha shughuli hii ya utiaji saini wenye heshima. Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya

Wete na pia Mwakilishi Mahsusi wa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, tunawashukuru sana kwa mchango wenu mkubwa. Tunaomba utufikishie shukrani zetu kwa Mkuu wa Mkoa.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Kitengo cha Millennium Challenge Account – Tanzania kimeanzishwa tarehe 21 Septemba 2007 ili kusimamia shughuli za miradi inayofadhiliwa chini ya Makubaliano (Compact) kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Marekani kupitia Shirika lake la Millennium Challenge Corporation (MCC)**.** Makubaliano hayo yalihitimishwa kwa kusainiwa na Marais wa pande zote mbili tarehe 17 Februari, 2008. Katika makubaliano hayo, MCA-T imepewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za miradi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayohusisha Sekta za Usafirishaji, Nishati na Maji Tanzania Bara na Zanzibar. Upatikanaji wa miradi inayohusika uliongozwa na malengo makuu chini ya MKUKUTA (Tanzania Bara) na MKUZA (Zanzibar).

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Mradi wa Ujenzi wa Barabara Tano za Vijijini Pemba ni mojawapo ya miradi iliyokubaliwa kutekelezwa katika sekta ya usafirishaji. Mradi huu unahusisha ujenzi hadi kufikia kiwango cha lami barabara tano zilizoko katika Mkoa wa

Kaskazini Pemba. Kwa kukoleza tu Barabara hizo zenye jumla ya urefu wa kilometa 35 ni:

1. Kipangani - Kangagani (Kilometa 2.7)
2. Chwale - Likoni (Kilometa 1.9)
3. Mzambarauni Takao – Pandani - Finya (Kilometa 7.9)
4. Mzambarauni Karimu – Finya - Mapofu (Kilometa 8.7) na
5. Bahanasa – Daya – Makongeni - Mtambwe (Kilometa 13.8)

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Mnamo tarehe 20 Novemba 2008, MCA-T ilisaini Mkataba wa Mashirikiano (Cooperation Agreement) na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, Zanzibar (sasa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano), kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Barabara hizo. Katika kipindi chote hadi sasa wataalamu wa Wizara wameifanya kazi yao kwa umahiri na umakini wa hali ya juu na wamekuwa bega kwa bega a wataalamu wa MCA-T na MCC na kutufikisha hapa tulipo leo na ni imani ya MCA-T kwamba tutaendelea kushirikiana kwa karibu zaidi katika awamu hii ngumu ya utekelezaji. Ni wazi kuwa wataalamu hao wasingeweza kuifanya kazi yao kwa kiwango walichoifanya pasipo miongozo, maelekezo na uwezeshwaji na Uongozi wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Hii ni pamoja na mashirikiano makubwa tuliyopata kutoka uongozi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba na Wilaya za Wete na Micheweni. Kwa

pamoja nawashukuruni sana kwa kuwa bega kwa bega nasi. Lengo letu sote ni kuona kuwa tunajenga barabara zinazoendana na viwango vilivyokubaliwa na kwa wakati.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Naomba sasa uniruhusu nitoe maelezo mafupi kuhusu historia ya mradi huu. Baadhi yetu tumekuwa tunajiuliza ni kwa nini Mkandarasi hakupatikana mapema zaidi kuliko ilivyo sasa. Mheshimiwa Mgeni Rasmi, kwa ufupi ni kuwa baada ya Mradi huu kuonekana kuwa unatimiza masharti ya awali ya uteuzi, kama ilivyo kwa miradi mingine, nyaraka zake ziliwasilishwa MCC kwa ajili ya zoezi la uhakiki wa taarifa zilizomo. Hii ilifuatiwa pia na ziara kadhaa katika maeneo ya mradi. Kubwa lililojitokeza ni kuwa mradi huu ulihusu zaidi barabara za vijijini tofauti na barabara kuu, na hivyo, kwa kutumia vigezo vya MCC wengi waliona kuwa barabara hizi hazingelistahili kuwa sehemu ya mradi mzima na kwa maana hiyo kustahili kuondolewa. Hata hivyo, baada ya mashauriano na majadiliano ya muda mrefu na ujengaji wa hoja kuhusu sifa za kipekee za barabara za vijijini Pemba, hatimaye tulikubaliana kwamba barabara hizi nazo zina sifa ya kujumuishwa kama sehemu ya miradi ya Tanzania. Katika hili tungependa kuwashukuru sana wenzetu wa MCC kwa kutuelewa.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Baada ya kupatikana kwa muafaka huo, hatua iliyofuata ilikuwa ni kuandaa upya upembuzi yakinifu (*feasibility study*), usanifu (*design*), athari za mazingira (EIA), mpango wa makaazi mbadala (*Resettlement Action Plan* - RAP*)* ambao ulijumuisha tathmini ya mali za wananchi watakaoathirika na ujenzi kwa ajili ya malipo ya fidia na matayarisho ya nyaraka za zabuni. Kampuni ya Intercontinental Consultants and Technocrats (ICT) Pvt. Ltd. ya India ilishinda zabuni kwa njia ya ushindani wa wazi kutayarisha nyaraka hizo.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Ni kutokana na mlolongo huu hatukuweza kulikamilisha zoezi la kumpata mkandarasi mapema kuliko sasa, lakini pia nataka kuwahakikishia kwamba ujenzi wa barabara zote utakamilika ndani ya muda tuliopewa na MCC. Tumepewa miaka mitano na tumebakiwa na miaka miwili. Kulingana na uchambuzi wa wataalamu kazi hii haitarajiwi kuchukua zaidi ya miezi 18, na hili ndilo litakalompa sifa Mkandarasi ambaye tutasaini naye mkataba hivi punde.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Kuanza kwa shughuli za ujenzi kunatanguliwa na maandalizi ya eneo la mradi na chini ya kanuni za MCC ni lazima maslahi

ya wananchi ambayo yanaguswa na mradi yapewe uzito unaostahili. Mradi hautokuwa na maana iwapo utekelezaji wake unawafanya wananchi wawe maskini zaidi kwa kukosa fidia stahilifu na hasa kwa ajili ya makaazi na mazingira mengine kwa ajili ya kuendeshea shughuli zao za maendeleo, elimu na ibada. Hivyo, utekelezaji wa Mpango wa Makaazi Mbadala ilibidi uandaliwe na kwa makini na malipo yalianza mwezi Mei 2011 na hadi hivi sasa wananchi 1,728 watakaoathirika na ujenzi wa barabara hizi sawa na asilimia 96 wameshalipwa fidia zao. Jumla ya TZS bilioni 3,972,085,000 zimeshalipwa au kutolewa na MCA-T. Kazi ya malipo kwa wananchi waliosalia ambao ni 73 sawa na asilimia 4 itakamilika ndani ya mwezi Agosti 2011. Pamoja na hatua hii nzuri iliyofikiwa ya kuwabaini na kuwaainisha waathirika bado kuna maeneo machache ya mashamba ambayo yameshafanyiwa tathmini na fedha zake kutengwa lakini wenyewe hawajajitokeza. Hivyo, katika hatua tuliyofikia, hatuna kisingizio chochote kile cha kutokumkabidhi Mkandarasi eneo la ujenzi ndani ya muda uliowekwa kisheria yaani siku 28 baada ya kuweka saini Mkataba.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Mafanikio tuliyoyapata katika utekelezaji wa zoezi la Mpango wa Makaazi Mbadala yametokana na kazi nzuri ya kupigiwa mfano iliyofanywa na viongozi wa Mkoa, Wilaya na vijiji na hasa napenda kuutambua kwa dhati kabisa mchango wa

Masheha 12 wa maeneo ya mradi na kwa utendaji wao ambao haukujali wakati. Hawa ni watu wenye imani kubwa, uaminifu na watu wasio na ubinafsi. Ninawashukuru sana na Mungu ataendelea kuwabariki katika kazi zao.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Katika zoezi la kumpata Mkandarasi tulikuwa na makampuni manne yaliyowasilisha zabuni zao ambayo ni China Railway Construction Engineering Group, Consolidated Contractors Group S.A.L (Offshore)- CCC ya Lebanon, H Young & Co. (East Africa) Ltd. ya Kenya na Spencon Services Ltd. ya Kenya. Baada ya kukamilika kwa zoezi la uchambuzi wa zabuni hizo na kwa kuzingatia vigezo vyote vilivyowekwa, kampuni ya H Young & Co. (East Africa) Ltd. ya Kenya iliibuka mshindi na ndio maana wako hapa leo. Wameshinda kihalali kabisa na sina mashaka nao.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Zoezi la kumpata Mhandisi Msimamizi wa Ujenzi nalo pia limeshakamilika. Kampuni ya LEA Associates Pvt, Limited ya nchini India ndiyo iliyoshinda zabuni na mkataba wake ulisainiwa tarehe 6 Julai 2011 mjini Dar es Salaam na kikanuni leo ndiyo inatakiwa ianze kuifanya kazi yake rasmi.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

MAENDELEO YA UTEKELEZAJI KWA MIRADI MINGINE

- Usafirishaji
- Nishati
- Maji

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Naomba sasa niipongeze rasmi kampuni ya H Young & Co. (East Africa) Ltd. ya Kenya kwa kuibuka mshindi na baada ya dakika chache tutasaini mkataba nayo. Kwa hivyo, baada ya leo tutachokuwa tunafuatilia ni maendeleo ya utekelezaji wa mkataba na jukumu kubwa la Mkandarasi ni kuhakikisha kwamba anafanya kazi kulingana na mkataba. Vile vile, ni lazima Mkandarasi awe karibu na wananchi anaowajengea barabara zao na viongozi wa Serikali wanaohusika. Pili, nawaomba wananchi wajue kuwa hizi ni barabara zao na kwa kufahamu hivyo wataweza kuhakikisha kwamba Mkandarasi anaifanya kazi yake kwa maelewano, amani na uaminifu. Ipo miradi ambayo imekufa kutokana na wafanyakazi na wananchi kubobea katika wizi na udokozi wa vitendea kazi vya Mkandarasi. Siamini kuwa mradi huu utapata matatizo haya kwa hapa Pemba. Ni mradi wenu wananchi na tunaomba mashirikiano yenu ili kwa pamoja tuweze kufikia malengo tuliyokusudia.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Baada ya kusema haya, naomba sasa nimalize kwa kuwashukuru sana sana kwa ushiriki wenu nyote katika tukio hili muhimu. Na mwisho kabisa nawatakieni pia muendelee vyema na mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhan.